

2024-02-15

‘Nzuri, na ya Kushangaza’: Msaidizi wa Usimamizi wa DSA Atuzwa kama Mtaalamu Bora wa Usaidizi wa Kielimu wa DCSD wa Mwaka

Cheo cha kazi cha Bi Donna Howard katika DeKalb School of the Arts (DSA) kinaweza kuwa “msaidizi wa usimamizi,” lakini kazi yake inajumuisha zaidi ya kusaidia tu usimamizi. Anategemewa kuwasaidia wafanyakazi wa shule, wanafunzi, wazazi, washirika wengine wa shule, na karibu chochote kingine kinachohitajika.

Kujitolea kwake kusaidia wengine kumefanya atuzwe kama Mtaalamu wa I wa Usaidizi wa Kielimu wa Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) kwa 2023-2024. Alikabidhiwa tuzo hiyo wakati wa Awamu ya 10 ya Tuzo za Kila Mwaka za Chuo cha Ubora wa Kielimu za Wilaya hii katika msimu uliopita wa mapukutiko na bado ameshangazwa kwa kutuzwa.

“Ninahisi kubarikiwa kupokea tuzo hii ya kifahari,” alisema. “Inanifanya nijisikie nimekamilika kutambuliwa kwa maadili yangu ya kazi na kujitolea kwa Shule za DeKalb.”

Bi. Howard alijiunga na DCSD mnamo mwaka wa 2007 kama karani wa habari wa shule ya msingi. Katika wakati huo, aliomba nafasi ya kujifunza shughuli za maktaba.

“Nilifurahia kufanya kazi na mtaalamu wa habari, wafanyakazi wote, na wanafunzi. Ninahisi sana jukumu hili liliniwezesha kujifunza na kuelewa kikamilifu majukumu na shughuli mbalimbali shuleni,” Bi Howard alisema. “Nachukulia kazi yangu ya karani wa habari kuwa hatua iliyoniwezesha kufikia hatua nyingine ndani ya wilaya.”

Baada ya kuhudumu kama karani wa habari kwa miaka kadhaa, akapewa kazi kama msaidizi wa usimamizi katika DSA na amefanya kazi huko kwa miaka 14 iliyopita. Alielezea shauku na kujitolea kwake kusaidia wengine kama sababu ya kutaka kuhudumu katika kazi hii.

“Naamini kwa uthabiti katika kuwatendea wengine kila mara kama ambavyo ungependa kutendewa,” Bi. Howard alisema. “Kila mtu anapaswa kutendewa kwa usawa na kwa heshima.”

Dkt. Keith Jones, Mwalimu Mkuu wa DSA, alimsifu Bi. Howard kama mfanyakazi mzuri ambaye shauku yake inaathiri vyema kila mtu anayehudumia.

“Bi. Howard ndiye gundi inayoshikilia pamoja taasisi hii ya kipekee. Uwepo wake huleta hisia nzuri, na ana sifa za kirafiki na kujiamini,” Dkt. Jones alisema. “Anatoa mwelekeo wazi wakati wa utata, maneno ya kutia moyo wakati wa masikitiko, na huwa kielelezo kila mara kwa wengine. Ana umuhimu sana kwa familia ya DSA.”

Kulingana na Bi. Howard, sehemu bora ya kufanya kazi katika DSA ni mazingira bora ya kazi. Alitaja kwamba wanafunzi mara nyingi hufika ofisini kwake kuimba, kucheza densi, kucheza mchezo wa kuigiza au kumjulia hali.

“Wasimamizi na wafanyakazi wa DSA hushirikiana pamoja kama timu ili kuhakikisha mafanikio ya wanafunzi,” aliongeza. “Ninapenda kwamba ingawa sote tuna majukumu yetu, tunashirikiana pamoja ili kuwahudumia wadau hawa wetu wa thamani - wanafunzi wetu.”

Bi. Howard alisema anatumai kazi yake inaonyesha maadili yake ya msingi ya wema, huruma na haki. Alishiriki kisa kimoja wakati mzazi aliuliza kuhusu jinsi anavyoendelea kuwa mchangamfu wakati wa siku ya shule. Alipojibu, alieleza kwamba kazi zake za kila siku na mwingiliano ni kielelezo tu cha sifa zake.

“Jukumu langu linaakisi sifa zangu, za DSA, na wilaya kwa ujumla,” alisema. “Ninajumuisha maadili yangu binafsi ninapowasiliana na kila mtu kila siku. Natumai maadili haya yatabaki daima.”

XXX